# HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

# MTIHANI WA KUJISOMEA NYUMBANI KWA DARASA LA SABA 2020

## SOMO: KISWAHILI

## MUDA: SAA 1:30 APRILI 2020,

**MAELEKEZO**

1.Karatasi hii ina sehemu A,B,C na D zenye jumla ya maswali **hamsini(50)**

2.Jibu maswali **yote** katika kila sehemu.

4.Andika **jina lako, wilaya, shule na somo kwa usahihi katika karatasi yako ya kujibia.**

### Sehemu A: Sarufi

Weka kivuli katika herufi ya jibu lililo sahihi zaidi katika karatasi yako ya kujibia

1. Katika neno "hatutakamilisha," kiambishi kinachoonesha nafsi ni kipi?
   (a) -ka- (b) -ta- (c) -ha- (d) -sha- (e) -tu-
2. Neno lima likinyumbulishwa katika kauli ya kutendeka litakuwa neno lipi?
   ( a ) limia, (b) limiana, (c) limika, (d) limisha, (E) limiana
3. Hasani alipata **munkari** jana alipokuwa akiangalia mpira baada ya timu yake kufungwa. Nini maana ya neno "munkari"

   (a) hamu (b) uzembe (c) jazba (d) ushabiki (e) husda

4. Neno harakati lina silabi ngapi?
   (a) moja (b) tatu (c) nane (d) sita (e) nne

5. Alfajiri na mapema tuliondoka ukumbini . Mzizi katika neno lililopigiwa mstari ni upi?
   (a) – ondo- (b) – iondoka (c) –ondok (d) ondoka (e) –iondok

6. Mwalimu mkuu wa shule____________mawazo ya wanafunzi katika kikao cha uongozi wa shule.
   (a) aliwakilisha (b) ariwasilisha (c) aliwasirisha (d) aliwasilisha (e) ariwasirishi

7. Walisema wao ni watoro. Neno lililotumika kama kiwakilishi ni ______________
   (a) ni (b) watoro (c) sana (d) walisema (e) wao.

8. Mwalimu alikuwa anatunga mtihani. Neno “anatunga” limetumika kama aina ipi ya kitenzi?
(a) kishirikishi (b) kitenzi kikuu (c) kisaidizi (d) kitenzi kipungufu (e) kitenzi jina

9. Wingi wa sentensi isemayo, “Ubao umetumika” ni upi” (a) mbao itatumika (b) mbao umetumika

(c) mbao zitatumika (d) mbao imetumika (e) mbao zimetumika.

10. Ni kipi kinyume cha neno “kaditama?”
(a) kati (b) mwanzo (c) chini (d) juu (e) mwisho

11. Kinyonga anaringa. Ukanushi wa sentensi hii ni (a) kinyonga haringi (b) kinyonga aringi
(c) kinyonga huringa (d) kinyonga hajaringa (e) vinyonga huringa.

12. Kisawe cha neno karai ni ________________

(a) bakuli (b) beseni (c) sufuria (d) pipa (e) ndoo

13. Kijiko kilichopotea kimepatikana hii ni aina gani ya sentensi?
(a) sahili (b) changamano (c) shurutia (d) huru (e) ambatano

14. <u>Kiazi</u> chake ni kitamu. Neno lililopigiwa mstari linapatikana katika ngeli ya ______________
(a) A – WA (b) U – YA (c) LI – YA (d) I – ZI (e) KI – VI

15. Katika maneno yafuatayo ni lipi ambalo ni nomino dhahania?
(a) unakuja (b) umeenea (c) utalima (d) uelewa (e) ulisoma

16. Joyce ameshinda Kondeni akiamia ndege. Kielezi katika sentensi hii ni_____________
(a) kondeni (b) akiamia (c) ameshinda (d) ddege (e) kondeni akiamia

17. Siku ya mahafali ilipo ________________ wanafunzi wote walienda ukumbini
(a) fika (b) wadia (c) tia nanga (d) aga (e) ingia

18. Katika sentensi zifuatazo ni ipi iliyo sahihi kimuundo?
(a) nilikwenda kituo cha afya nilimkuta daktari hayupo
(b) nilikwenda kituo cha afya lakini nilimkuta daktari hayupo
(c) nilikwenda kituo cha afya lakini sikumkuta daktari
(d) nilipokwenda kituo cha afya nikamkuta daktari hayupo
(e) nilipokwenda nikamkuta hayupo.

19. “Mvua ilinyesha jana usiku kucha”. Katika sentensi hii kikundi kielezi ni kipi?
(a) mvua ilinyesha jana (b) usiku kucha (c) ilinyesha jana (d) mvua ilinyesha (e) jana usiku kucha

20. Kisawe cha neno “bahati” ni kipi kati ya maneno yafuatayo?

(a) tunu (b) sudi (c) shani (d) hiba (e) hidaya

## Sehemu B: Lugha ya Kifasihi

21. Methali ipi inapingana na ile isemayo"haba na haba hujaza kibaba"
    (a) chembe na chembe mkate huwa (b) wastara haumbuki (c) tembea uone

    (d) chovya chovya humaliza buyu la asali (e) dawa ya moto

22. Kiangazi chote hulala usingizi: yakija masika anakesha. maana yatendawili hiki ni ipi?
    (a) nyoka (b) kaa (c) samaki (d) ndege (e) chura
23. Watu wametega sikio kujua kitakachotangazwa. Neno "Wametega sikio" lina maana gani?
    (a) panua masikio (b) zibua masikio (c) fungua masikio yote
    (d) sikiliza kwa makini (e) ambiana waziwazi

24. Anika juani maana ya nahau hii ni ________
    (a) tega sikio (b) kaa chonjo (c) fuja mali (d) toa siri (e) vunja mbavu.

25. "Ntandu alikuwa na kichwa cha panzi". Msemo " kichwa cha panzi " una maana ipi?
    (a) msikivu sana (b) msahaulifu sana (c) ana utambuzi (d) ana kumbukumbu (e) mtiifu sana

26. Nikitembea waliowafu huniamkia na walio hai hukaa kimya maana ya kitendawili hiki ni __________
    (a) nyuki walio ndani na nje ya mzinga (b) yai na kifaranga (c) majani makavu na mabichi (d) kulala usingizi na kuamka (e) tumbo la binadamu linaponguruma.

27. Wanafunzi wa darasa la sita wanafanya kazi zote <u>bega kwa bega</u>. Neno lililopigiwa mstari lina maana gani?
    (a) kuwasilishana (b) kuegemeana (c) kutegeana (d) kushirikiana (e) mabega mawili

28. Alikubali kwa ulimi ina maana kuwa ___________
    (a) kutoa kauli kali (b) aliitikia kwa kutumia ulimi (c) kukubali kwa maneno (d) kupiga kelele
    (e) kukataza

29. Hausimami hausimiki, jibu la kitendawili hiki ni lipi?
    (a) kobe (b) mkuki (c) nati (d) mkufu (e) moto

30. " Akutendaye mtende usimche akutendaye" Methali hii inatoa funzo gani?.
    (a) mwovu akomeshwe kwa adhabu kali (b) akufanyiae maovu usimche (c) anayekutendea usilipize kisasi (d) mwovu akwepwe kwa kutenda (e) mwovu akwepwe kwa kutendwa

## Sehemu C: Ufahamu

**Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata chini yake kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuweka kivuli herufi ya jibu hilo kwenye karatasi ya kujibia uliyopewa.**

Mabadiliko ya hali ya hewa yamekuwa makubwa kiasi cha kutisha . Zamani mababu zetu walitabiri mvua wao wenyewe pasi na kuwa na vyombo vya kisasa. Suala linalozungumziwa sana siku hizi ni mabadiliko ya hali ya hewa na athari zake kwa jamii nzima. Kila mtu anawasiwasi kuhusu mvua ambazo huchukua muda bila kunyesha.

Ukosefu wa mvua ambao mwishowe huleta ukame na njaa umechangiwa kwa kiasi kikubwa na shughuli za binadamu ambazo zinaongezeka kwa haraka siku hadi siku. Shughuli hizo mbalimbali ambazo kwa upande mmoja zinaonekana kama za kimaendeleo ni kuongezeka kwa matumizi ya maliasili. Mifano mbalimbali ambayo inaonesha matumizi hayo ni pamoja na ujenzi wa nyumba zaidi kupata nishati ya kutosha kwa ajili ya kupitia na upatikanaji wa mbao na magongo kwa wingi kwa matumizi ya ndani na hata ya nje ya nchi.

Hata hivyo ili maendeleo yawe na mwelekeo chanya kijamii inalazimika kupanda miti kwa wingi ili kukidhi mahitaji hayo. Aidha ni vema kuzingatia kuwa ukataji miti ni chanzo kikubwa cha mito na vijito kuwa na maji haba au kukauka kabisa.

**Maswali**

31. Kichwa cha habari kinachofaa kwa habari hii ni kipi?
    (a) mabadiliko ya hali ya hewa (b) ukosefu wa chakula (c) kuongezeka kwa joto (d) kuongezeka kwa ukame (e) mabadiliko ya hali ya hewa na athari zake

32. Mwandishi anaeleza mabadiliko ya hali ya hewa kuwa yalikuwa___________
    (a) hayakadiriki (b) ya hali ya juu (c) ya kutisha (d) ya kukadirika (e) hayatabiriki

33. Tatizo kubwa zaidi ambalo husababishwa na ukosefu wa mvua kwa muda mrefu ni lipi kati ya haya yafuatayo:-

    (a) kukatika kwa umeme (b) Ujenzi kupungua (c) kukosekana nishati (d) kukosekana kwa miti

    (e) kuwepo kwa baa la njaa

34. Neno haba kama lilivyotumika katika habari hii lina maana gani?
    (a) kidogo (b) kiasi (c) kadri (d) wastani (e) rasharasha

35. Kisawe cha neno mwishowe kama lilivyotumika katika habari hii ni kipi?
    (a) tamati (b) hatima (c) baadaye (d) hatimaye (e) hitimisho
36. Mabadiliko ya hali ya hewa yana maana sawa na ipi kati ya hizi zifuatazo:-
    (a) uoto (b) jotoridi (c) mazingira (d) sura ya nchi (e) tabia ya nchi
37. Watu wa zamani waliweza kutabiri mvua kwa kutumia ___________
    (a) vyombo vya kisasa (b) kipajii chao wenyewe (c) vyombo vya zamani
    (d) kipima mvua cha kienyeji (e) ubunifu waliorithi

38. Mito na vijito huwa na maji haba au kukauka kutokana na nini?

(a) kukata mali kwa wingi (b) kuchoma majani karibu na mito
(c) Kukata majani kwa wingi (d) Kuchoma na kukata miti iliyozunguka mito

(e) kupanda miti kuzunguka vijito

39. Nishati ni neno lenye maana sawa na lipi?
(a) kawa (b) kivo (c) kiwi (d) kivi (e) kawi

40. Dalili mojawapo kubwa ya maendeleo ni ipi kama inavyoelezwa katika kifungu cha habari?
(a) kupata nishati ya kupikia (b) ongezeko la miti ya kujengea (c) ongezeko la utumiaji wa maliasili (d) upatikanaji wa mbao na magongo (e) ongezeko la ujenzi wa nyumba

## Sehemu D: Ushairi

Soma kwa makini shairi lifuatalo kisha jibu maswali yaayofuata kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi

1. Wapende baba na mama, upate zao baraka,
Dunia uone njema, uishi pasi na shaka,
Usiachiwe lawama, na mwisho kulaanika,
Ili upate baraka, heshimu baba na mama

2. Wazazi wana huruma, kuwatukuza hakika,
Uwape yao heshima, ili upate Baraka,
Ukiitwa nenda hima, **rabeka** kuwaitikia,
Ili upate baraka, heshimu baba na mama

3. Heshimu baba na mama, kiburi kukiepuka,
Baba umpe heshima, mama naye kadhalika,
Ukigombana na mama, laana taku**gubika,**
Ili upate baraka, heshimu baba na mama

**Maswali**

41. Shairi hili lina beti ngapi? ___________

42. Kina cha kati ni ______________

43. Shairi lina mizani mingapi? __________

44. Maana ya neno gubika ni _____________

45. Kituo katika shairi hili ni____________________________________